Sala Ni Nguzo Ya Dini

Sala Ni Nguzo Ya Dini

Mustafa Ranjbar Shirazi

Kimetafsiriwa na
Ibrahim Khamisi

Al-Islam.org

Author(s):

Mustafa Ranjbar Shirazi [1]

Publisher(s):

Al-Itrah Foundation [2]

Sala ni nguzo kubwa ya dini. Mtukufu Mtume (s.a.w.) amesema: "Sala ni nguzo ya dini, mwenye kuivunja ameivunja dini, na mwenye kuisimamisha ameisimamisha dini." Mtukufu Mtume ameongeza: "Kila kitu kina uso, na uso wa Uislamu ni sala. Mwenye kuacha kusali ameuchafua uso wa dini." Imam Muhammad Baqir (a.s.) amemnukuu Mtukufu Mtume (s.a.w.) akisema: "Kitu cha kwanza atakachohesabiwa muumini (Siku ya Kiyama) ni Sala. Ikikubaliwa yatakubaliwa matendo mengine, na ikikataliwa yatakataliwa matendo mengine pia."

Kwa ufupi, kuna hadithi nyingi sana kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.) na Maimamu (a.s.) kuhusu umuhimu wa Sala kiasi kwamba katika hadithi moja, Mtukufu Mtume (s.a.w.) amesema kwamba kitu chenye kutofautisha baina ya Uislamu na ukafiri ni Sala.

Wakati huu tulionao una mitihani mingi sana, vijana wa Kiislamu na wazee pia wamejitumbukiza katika vitendo viovu na vichafu kiasi kwamba mtu hawezi kumtofautisha na mnyama, na pengine hata mnyama ni afadhali. Ili kuishinda mitihani hii na maovu haya, dawa yake ni kushikamana na Sala. Allah 'Azza wa Jalla anasema katika Qur'ani Tukufu: "... Hakika Sala huzuia mambo machafu na maovu, na kwa hakika kumbuko la Allah ni (jambo) kubwa kabisa, na Allah anajua mnayoyatenda." (29:45)

Get PDF [3] Get EPUB [4] Get MOBI [5]

Translator(s):

Ibrahim Khamisi [6]

Topic Tags:

Salah (Prayers) [7]

Neno La Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako ambacho ndani yake Sala (swala) imeelezwa pamoja na vielelezo vya picha, tumekiita: Sala ni Nguzo ya Dini. Sala ni nguzo kubwa ya dini. Mtukufu Mtume (s.a.w.) amesema:

"Sala ni nguzo ya dini, mwenye kuivunja ameivunja dini, na mwenye kuisimamisha ameisimamisha dini." Mtukufu Mtume ameongeza: "Kila kitu kina uso, na uso wa Uislamu ni Sala.

Mwenye kuacha kusali ameuchafua uso wa dini." Imam Muhammad Baqir (a.s.) amemnukuu Mtukufu Mtume (s.a.w.) akisema: "Kitu cha kwanza atakachohesabiwa muumini (Siku ya Kiyama) ni Sala. Ikikubaliwa yatakubaliwa matendo mengine, na ikikataliwa yatakataliwa matendo mengine pia."

Kwa ufupi, kuna hadithi nyingi sana kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.) na Maimamu (a.s.) kuhusu umuhimu wa Sala kiasi kwamba katika hadithi moja, Mtukufu Mtume (s.a.w.) amesema kwamba kitu chenye kutofautisha baina ya Uislamu na ukafiri ni sala. Wakati huu tulionao una mitihani mingi sana, vijana wa Kiislamu na wazee pia wamejitumbukiza katika vitendo viovu na vichafu kiasi kwamba mtu hawezi kumtofautisha na mnyama, na pengine hata mnyama ni afadhali. Ili kuishinda mitihani hii na maovu haya, dawa yake ni kushikamana na sala. Allah 'Azza wa Jalla anasema katika Qur'ani Tukufu: "... Hakika Sala huzuia mambo machafu na maovu, na kwa hakika kumbuko la Allah ni (jambo) kubwa kabisa, na Allah anajua mnayoyatenda." (29:45)

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan katika wakati huu ambapo jamii inazidi kudidimia katika maovu kutokana na kumomonyoka kwa maadili mema. Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru mwandishi wa kitabu hiki, Mustafa Ranjbar Shirazi, na ndugu yetu Ibrahim Khamisi kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha uchapishaji wa kitabu hiki.

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation
S. L. P. 1017
Dar-es-Salaam.

Dibaji

“Mola wangu Mlezi! nijaalie niwe msimamishaji Swala na kizazi changu, Mola wetu! na upokee maombi yangu”1

Himidi zote zinamstahiki Mwenyezi Mungu, kisha rehma na amani ziwe juu ya mjumbe wa Allah na kizazi chake kitakasifu kitoharifu.

Utumishi wa mja kwa Mwenyezi Mungu ndiyo lengo la kila amali, na Swala ndiyo nyenzo yake, kwani ni

ngazi ya muumini na ni nguzo miongoni mwa nguzo za Uislamu. Anasema Imam Al-Baqir (a.s): “Kitu cha kwanza atakachohesabiwa muumini (Siku ya Kiyama) ni Swala, ikikubaliwa yatakubaliwa matendo mengine, na ikikataliwa basi yatakataliwa matendo mengine.”2

Kutokana na ukweli huu, tumeonelea vyema kukipa kizazi chipukizi fursa ya kuyatambua yale yanayokihusu kwa kutoa mfululizo wa sheria kwa njia rahisi na maudhui nyepesi kufahamika, kwa kuweka kitabu maalumu chenye picha zinazofafanua mada na kumuonyesha mpendwa msomaji namna ya kutekeleza ibada na taratibu zake kwa njia nyepesi na rahisi.

Kitabu hiki tumekiita Swala ni nguzo kuu ya dini. Tunamuomba Mola Mtukufu akifanye kitabu hiki kiwe chenye manufaa kwa Waislamu, na hasa vijana wa umma huu ambao ndio tegemeo la mustakabali wake, na atukubalie kazi yetu hii ndogo katika kuitumikia dini Yake tukufu.

Ewe Mola wetu! Tukubalie, hakika Wewe ni Msikivu, Mjuzi.

Mustafa Ranjibar Shiraz.
E: mail: ranjbar85@yahoo.com [8]

1. Sura Ibrahim: 40
2. Biharul-An'war, Juz. 47 Uk. 2.

Utangulizi

Amesema Allah Mtukufu: “Na sikuumba majini na watu ila wapate kuniabudu.”1

Ustaarabu wa Kiislamu umetokana na mafunzo mazuri ya dini ya Kiislamu na umesaidia kuratibu maswala ya dini na dunia, hivyo Uislamu ni dini ya imani na sharia. Ni dini ya maendeleo na mafanikio kwa kila aina zake.

Mizizi Ya Dini:

Dini ni mkusanyiko wa imani na majukumu ya kivitendo yaliyoletwa na Manabii kutoka kwa Mwenyezi Mungu ili kuwaelekeza na kuwaongoza wanadamu. Hivyo nafsi kujengeka katika msingi wa imani hizi huku ikitekeleza majukumu haya ya kivitendo ndiyo sababu ya mwanadamu kufanikiwa kwa wema ndani ya maisha haya ya Dunia na Akhera, hivyo mizizi hiyo ya dini ni mitano:

I. Tawhidi:

Ni kuamini kuwa ulimwengu una Mungu aliyeuumba na kuufanya uwepo baada ya kuwa haukuwapo, na

kwamba huyo Muumba wa ulimwengu ni Mmoja Mpekee asiyekuwa na mshirika.

II. Uadilifu:

Ni kuamini kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ni mwadilifu, hamdhulumu yeyote, na kwamba matendo Yake yana hekima, hivyo, hatendi chochote isipokuwa kina masilahi kwa viumbe.

III. Utume:

Ni kuamini kuwa Mwenyezi Mungu hawaachi viumbe wake bila mwongozo, hivyo aliwatuma manabii ili wawaite watu kwenye njia iliyonyooka. Na Nabii wa kwanza ni Nabii Adam (a.s) na wa mwisho ni Nabii Muhammad (s.a.w.w), na kwamba dini ikubaliwayo kwa Mwenyezi Mungu ni Uislamu na ndio dini kamili.

IV. Uimamu:

Ni kuamini kuwa, kama ambavyo Mwenyezi Mungu aliteua Manabii na mitume, vivyo hivyo aliteua warithi wa Mitume yake. Ili kuendeleza kazi ya unabii wa bwana wetu Muhammad (s.a.w.w.) aliwateua Maimamu, warithi na Makhalifa kumi na wawili, wa kwanza wao ni Ali bin Abi Twalib (a.s) na wa mwisho ni Imam Al-Mahdi (a.t.f.s).

V. Marejeo:

Ni kuamini kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu atawafufua watu baada ya kifo ili kumlipa mtiifu kwa wema na kumwadhibu aliyeasi, ili awape malipo ya kudumu.

Matawi Ya Dini:

Ni hukumu alizoziweka Allah Mtukufu kupitia Qur'an na Sunna tukufu kwa masilahi ya waja wake, na ambazo Mtume (s.a.w.w.) ametulingania kuzifuata, na akatuamuru kuzitekeleza, zikiwa na lengo la kuzitoharisha nafsi na kuimarisha utumishi wake kwa Allah Mtukufu. Matawi ya dini yaliyo muhimu zaidi ni:

1. **Swala**
2. **Saumu**
3. **Zaka**
4. **Hijja**
5. **Khumsi**

6. **Jihadi**

7. **Kuamrisha mema na kukataza maovu**

8. **Kumtawalisha Mtume (s.a.w.w.) na Ahlul-Bayti wake watoharifu (a.s) na kujiepusha na adui zao.**

1. Sura Adh-Dhariyyat: 51.

Swala

Ni matendo na maneno ambayo hujenga mahusiano kati ya Muumba na kiumbe, hivyo mja akiikata, basi mawasiliano yake na Mola wake hukatika.

Allah Mtukufu anasema: "Kwa hakika Mimi ndiye Mwenyezi Mungu hakuna aabudiwaye ila Mimi tu, basi niabudu na simamisha Swala kwa kunitaja."1

Thamani Ya Swala Ndani Ya Uisilamu:

Swala huchukuliwa kuwa miongoni mwa mambo ya dharura zaidi ya Uisilamu na nguzo zake. Imepokewa kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) kuwa alisema:

"Swala ni nguzo ya dini, ikikubaliwa matendo mengine hukubaliwa, na ikikataliwa na matendo mengine hukataliwa"2

Daraja hii kubwa ya sala ndiyo tunayoiona katika Aya za Qur'an na Hadithi Tukufu, ikiwemo:

I. Kudumisha Swala Ni Miongoni Mwa Sifa Muhimu Za Waumini:

"Hakika wamefuzu wenye kuamini. Ambao ni wanyenyekevu katika Swala zao".3
"Na ambao Swala zao wanazihifadhi."4

II. Kutekeleza Swala Ni Miongoni Mwa Sababu Za Udugu Wa Kiislamu:

"Na kama wakitubu na wakasimamisha Swala na wakatoa Zaka, basi ni ndugu zenu katika dini ..."5

III. Kusimamisha Swala Ni Miongoni Mwa Sifa Za Jamii Bora:

"Wale ambao tukiwapa madaraka katika nchi husimamisha Swala na hutoa Zaka na huamrisha yaliyo mema na hukataza yaliyo mabaya, na kwa Mwenyezi Mungu ndiko mwisho wa mambo".6

IV. Swala Ni Nyenzo Ya Mafanikio:

“Hakika amekwishafaulu aliyejitakasa. Na akakumbuka jina la Mola wake na akaswali.”7

V. Kuwaelimisha Watoto Swala Ni Katika Majukumu Ya Wazazi:

“Na waamrishe watu wako kuswali, na uendelee kwa hayo, hatukuombi riziki bali Sisi tunakuruzuku, na mwisho mwema ni kwa mcha Mungu.”8

VI. Swala Ni Katika Nguzo Za Dini:

“Wala hawakuamrishwa ila kumwabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtaka– sia yeye dini, hali wameshikamana na haki, na wanasimamisha Swala na kutoa Zaka, na hiyo ndiyo dini madhubuti.”9

VII. Swala Ni Shukurani Kwa Mneemeshaji:

“Hakika Sisi tumekupa kheri nyingi.* Basi sali kwa ajili ya Mola wako, na uchinje.* Hakika adui yako ndiye aliyekatikiwa kizazi”10

Athari Za Swala Na Siri Zake:

I. Huleta Utulivu Wa Nafsi

“Kwa hakika binadamu ameumbwa hali ya kuwa mwenye pupa.* Inapomgusa shari huwa mwenye fazaa.* Na inapomgusa kheri huwa anaizuilia.* Ila wanaosali.”11

II. Ni Kinga Ya Muumini

“Na ombeni msaada kwa subira na Swala na kwa hakika jambo hilo ni gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu.”12

III. Swala Ni Njia Ya Mafanikio Na Ukamilifu

“Na simamisha Swala katika sehemu mbili za mchana na nyakati za usiku hakika mema huyaondoa maovu, huo ndio ukumbusho kwa wenye kukumbuka.”13

“…Bila shaka Swala huzuia mambo machafu na maovu…”14

IV. Swala Humfundisha Binadamu Mipango Na Nidhamu Katika Maisha

“…Hakika Swala kwa wenye kuamini ni faradhi iliyo na wakati maalumu.”15

Hukumu Za Swala

Ili kutekeleza Swala ambayo humaanisha kuhudhuria mbele ya Mungu wa ulimwengu na kudhihirisha utumwa na utii kwake, ni lazima vikamilike vitangulizi ambavyo ni lazima kuvitimiza kabla ya sala na ndani yake, huku ukiviambatanisha na mambo ya wajibu, na muda huohuo ukijiepusha na vibatilishi vyake.

Vitangulizi Vya Swala

Tohara: Hali hii imegawanyika sehemu mbili:

a) Tohara dhidi ya najisi: Nayo ni hali ya mwili na mavazi ya mwenye kusali kuwa tohara dhidi ya najisi.

b) Tohara dhidi ya hadathi: Nayo ni hali ya mwenye kusali kuwa na tohara yakimaana (ya ndani) huku akikusudia kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu kupitia udhu au kuoga au tayammam.

Tohara hii ya pili ina hali mbili:

Ya kwanza: Wakati wa kupatikana maji: Wakati huo inawezekana kupata tohara kwa moja kati ya mambo mawili:

a. Udhu.

b. Kuoga kunakotosheleza udhu (Kama vile kuoga janaba).

Ya pili: Wakati wa kukosekana maji: Wakati huo inawezekana kupata tohara kwa njia ya kutayammamu (badala ya udhu na josho).

Mavazi ya mwenye kusali: Ni vile ambavyo mwenye kusali kuvitumia kuusitiri mwili wake na utupu wake wakati wa kusali.

Mahali pa kusalia: Ni mahali pa kutekelezea sala, ambapo ni sharti pawe pa halali. Vilevile mahali pa kusujudia pawe tohara.

Nyakati za Swala: Nazo ni zile nyakati zilizoainishwa na sharia kwa kila Swala ya faradhi.

Kibla: Ni upande wa Al-Kaaba tukufu ambayo mwenye kusali anataki- wa aelekeze uso wake na mwili wake wakati wa kusali.

1. Sura Twaha: 14.
2. Biharul-An'war, Juz. 47 Uk. 2.
3. Sura Al-Muuminun: 1 - 2.
4. Sura Al-Muuminun: 9.
5. Sura At-Tawba: 11.

6. Sura Al-Haji: 41.
7. Sura Al-Aaala: 14 - 15.
8. Sura Twaha: 132.
9. Sura Al-Bayyinah: 5.
10. Sura Al-Kawthar.
11. Sura Al-Maarij: 19 - 22.
12. Sura Al-Baqarah: 45.
13. Sura Hud: 114.
14. Sura Al-Ankabut: 45.
15. Sura An-Nisai: 103.

Udhu

Mwenyezi Mungu amesema: “Enyi mlioamini! Mnaposimama kwa ajili ya Swala, basi osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu na miguu yenu mpaka vifundoni. Na mkiwa na janaba, basi ogeni. Na mkiwa wagonjwa au safarini, au mmoja wenu ametoka chooni au mmeingiliana na wanawake, na hamkupata maji, basi tayamamuni mchanga ulio safi na mpake nyuso zenu na mikono yenu Mwenyezi Mungu hapendi kukutieni katika taabu, lakini anataka kukutakaseni na kutimiza neema Yake juu yenu ili mpate kushukuru.”1

Ni Wakati Gani Tunawajibika Kisharia Kuwa Na Udhu?

i. Ni lazima kuchukua udhu kwa ajili ya kila Swala ya faradhi au ya sunna isipokuwa sala ya kumsalia maiti, kwani si lazima kuchukuwa udhu kwa ajili yake.

ii. Kwa ajili ya kuizunguka Al-Kaaba wakati wa ibada ya Hijja na Umra.

iii. Kwa ajili ya kugusa maandishi ya Qur’an Tukufu.

Masharti Ya Kusihi Kwa Udhu

i. Nia ya kujikurubisha kwa Allah Mtukufu

ii. Maji yawe tohara

iii. Yawe maji halisia: Yaani yasiwe maji ya matunda au yaliyokamuliwa toka kwenye mmea wowote ule (Kama vile maji ya waridi), au yaliyochanganywa na mada yoyote ile (kama vile maji ya sabuni, maji ya iriki au soda).

iv. Yawe maji ya halali: Yaani yasiwe maji ya wizi, na unyang’anyi au yatokanayo na kipato kisicho cha halali kisharia.

v. Chombo cha udhu kiwe cha halali: Yaani kisiwe cha wizi na unyang'anyi au kitokanacho na kipato kisicho cha halali kisharia.

vi. Chombo cha kufanyia udhu kisiwe cha dhahabu au fedha. vii. Viungo vya udhu viwe tohara.

vii. Kuwepo na muda utoshao kufanya udhu na kusali.

viii. Utaratibu baina ya viungo vya udhu: Yaani aoshe uso kwanza kisha mkono wa kulia na kisha wa kushoto, na baada ya hapo apake kichwa na kisha miguu yake miwili.

ix. Mfululizo baina ya viungo vya udhu: Yaani wakati wa kuchukua udhu asipitishe muda mrefu kabla ya kwenda kiungo kingine kwa kiasi ambacho itapelekea kukauka kwa viungo vya mwanzo kabla ya udhu kukamilika.

x. Atende matendo ya udhu yeye mwenyewe, na wala mtu mwingine asimfanyie udhu, isipokuwa katika hali ya dharura. (Hii ina maana kwamba, kama ukimwambia mtu akuoshe uso na mikono n.k. udhu wako utabatilika; lakini kama huwezi kufanya udhu mwenyewe kwa sababu za ugonjwa unaweza kuomba msaada kwa mtu mwingine).

xi. Lisiwepo tatizo au hatari yoyote ile iwezayo kutokea kutokana na kutumia maji, kama vile maradhi, hofu ya kiu, au kuihofia nafsi yake au nafsi yenye kuheshimika.

xii. Kisiwepo kizuizi chochote katika viungo vya udhu kinachoweza kuzuia maji kugusa ngozi, kama vile mafuta na rangi.

xiii. Kichwa na miguu viwe vikavu kabla ya kupaka maji.

1. Sura Al-Maidah: 6.

Jinsi Ya Kutawadha

Kwanza: Nia: Nayo ni kukusudia moyoni kuwa: Ninatawadha kwa ajili ya kutafuta radhi ya Allah. Baada ya hapo anza kutenda matendo yafuatayo huku ukiendelea kuwa na nia hiyo moyoni.



Pili: Kuosha uso kwa kutumia mkono wa kulia, kuanzia kwenye maoteo ya nywele za kichwa mpaka kwenye ncha ya kidevu. Na ni lazima kuosha kuanzia juu kwenda chini kama inavyoonekana katika picha nambari (1) na (2).

Wakati wa kuosha uso ni sunna kusoma dua ifuatayo:

اللهُمَّ بَيِّضْ وَ جْهِيْ يَوْمَ تَسْوَدَّ فِيْهِ الوُجُوْهُ وَ لاَ تُسَوِدَّ وَ جْهيْ يَوْمَ تَبْيَضُّ فِيْهِ الوُجُوْهُ

Allahumma! Bayyidh Wajhi yawma tas'waddu fiyhil Wujuuhu walaa tusawwid wajhi yawma tabyaddhu fiyhil wujuuhu

"Ewe Mwenyezi Mungu! ung'arishe uso wangu Siku ambayo nyuso zitafifia, na usiufifize uso wangu Siku ambayo nyuso zitang'ara."

Tatu: Kuosha mkono wa kulia kuanzia kwenye kifundo mpaka kwenye ncha za vidole. Na ni lazima kuosha kuanzia juu kwenda chini kama inavyoonekana katika picha nambari (3) na (4).

Wakati wa kuosha mkono wa kulia ni sunna kusoma dua ifuatayo:

اللهُمَّ أعْطِنِي كِتاَ بي بيَمِيْنِيْ وَ اَلخُلْدَ فِي الجِنَان بيَسَاري وَ حَا سِبْنِي حِسَابًايَسِيْرًا

Allahumma Aatwini kitaabi biyamiyni, walkhulda fil jinaan biyasaari, wahaasibni hisaban Yasiira
"Ewe Mwenyezi Mungu! unipe kitabu cha hesabu ya matendo yangu kwa mkono wangu wa kulia, na kuishi kwa mkono wangu wa kushoto."

Nne: Kuosha mkono wa kushoto kuanzia kwenye kifundo mpaka kwenye ncha za vidole. Ni lazima kuosha kuanzia juu kwenda chini. kama inavyoonekana katika picha nambari (5) na (6).

Wakati wa kuosha mkono wa kushoto ni sunna kusoma dua ifuatayo:

اللهُمَّ لاَ تُعْطِنِيْ كِتَا بِي بشِمِالِي وَلاَ تَجْعَلْهَا مَغْلُوْلَة اِلَي عُنُقِي

Allahumma la tuutwini kitaabi bishimali, walaa taj'alha maghlulatan ilaa unuqii
"Ewe Mwenyezi Mungu! usinipe kitabu cha matendo yangu kwa mkono wangu wa kushoto na usiufanye kuwa wenye kujikunja shingoni mwangu.

Tano: Kupaka kichwa sehemu ya mbele kwa mkono wa kulia kutumia unyevunyevu wa udhu uliobaki kwenye kiganja. Usichukue maji mengine tofauti na unyevunyevu uliyobaki kwenye mkono, kama inavyoonekana katika picha nambari (7) na (8).

Wakati wa kupaka maji kichwani, ni sunna kusoma dua ifuatayo:

اللهُمَّ غَشِّنِيْ برَ حْمَتِكَ وَ بَرَ كَا تِكَ وَعَفْوِكَ

Allahumma Ghas-Shini birahmatika wa barakaatika wa afwika
"Ewe Mwenyezi Mungu nifunike kwa rehma, baraka na msamaha Wako."

Sita: Kupaka juu ya unyayo wa kulia kwa kiganja cha mkono wa kulia, kuanzia kwenye ncha za vidole hadi kwenye kifundo cha mguu, ukitumia unyevunyevu wa udhu uliobaki mkononi, kama inavyoonekana katika picha nambari (9) na (10).

Wakati wa kupaka miguu ni sunna kusoma dua ifuatayo:

اللهُمَّ ثَبِّتْنِي عَلَي الصِرَاطِ يَوْمَ تَزُلَّ فِيْهِ الأَ قْدَامُ وَاجْعَلْ سَعْيِي فِيْمَا يُرْضِيْكَ عّنِي

Allahummah thabbitni ala swiraat yawma tazallu fiyhil aqdaam, waj'al saa'yi fiyma yurdhika anni

"Ewe Mwenyezi Mungu nithabitishe juu ya njia siku ambayo nyayo zitateleza, na ujaalie harakati zangu ziwe katika yale yakuridhishayo."

Saba: Kupaka juu ya unyayo wa kushoto kwa kiganja cha mkono wa kushoto, kuanzia kwenye ncha za vidole hadi kwenye kifundo cha mguu, ukitumia unyevunyevu wa udhu uliobaki mkononi, kama inavyoonekana katika picha nambari (11) na (12).

Wakati wa kupaka miguu ni sunna kusoma dua ifuatayo:

اللهُمَّ ثَبِّتْنِي عَلَي الصِرَاطِ يَوْمَ تَزُلَّ فِيْهِ الأَ قْدَامُ وَاجْعَلْ سَعْيِي فِيْمَا يُرْضِيْكَ عّنِي

Allahummah thabbitni ala swiraat yawma tazallu fiyhil aqdaam, waj'al saa'yi fiyma yurdhika anni
"Ewe Mwenyezi Mungu nithabitishe juu ya njia siku ambayo nyayo zitateleza, na ujaalie harakati zangu ziwe katika yale yakuridhishayo."

Vinavyotengua Udhu

i. Kutokwa na mkojo na kile kilicho chini ya hukumu yake, kama vile unyevunyevu utokao kabla ya kufanya istibraa.[1]

ii. Kutokwa na haja kubwa.

iii. Kutokwa na upepo katika sehemu ya kawaida.

iv. Usingizi wenye kuvighilibu via vya usikivu na uono.

v. Kila kinachoondoa akili, kama vile ulevi, wendawazimu au kuzimia.

vi. Kila kinachowajibisha kuoga, kama vile janaba, kugusa maiti, ambavyo huitwa hadathi kubwa.

Mambo Ya Sunna Katika Udhu

Ni sunna kabla ya kufanya udhu kutenda yafuatayo:

i. Kuosha mikono mpaka kwenye kiwiko.

ii. Kusukutua maji kinywani mara tatu, au angalau mara moja. iii. Kuingiza maji puani mara tatu, au mara moja kwa uchache.

iii. Kuomba dua zilizopendekezwa kwa kila kiungo cha udhu. Dua hizo zimeshatangulia kwenye maelezo ya jinsi ya kutawadha.

Udhu Wa Bandeji (Jabira)

Udhu wa Bandeji (Jabira)– Neno Bandeji hapa linamaanisha chochote kile kinachowekwa kwenye jeraha kitabibu, sawa iwe bandeji ya kawaida au plasta au kitambaa au pamba na vinginevyo– **Mhariri.**

Ikiwa kwenye moja ya viungo vya udhu kuna bandeji iliyosababishwa na jeraha, jipu au kuvunjika, basi kukiwa na uwezekano wa kuiondoa bandeji italazimu kufanya hivyo, na kama haiwezekani basi atapaka juu yake, kama inavyoonekana katika utaratibu wa kisharia ufuatao:

I. Ikiwa Kiungo Chenye Jeraha Ni Uso Au Mkono Na Kiungo Hicho Kikawa Wazi Bila Bandeji:

a. Ikiwa maji hayatamletea madhara basi atafanya udhu wake kwa utaratibu wa kawaida.

b. Ikiwa maji yatamletea madhara na inawezekana kuosha pembezoni mwa jeraha basi itatosha kufanya hivyo. Na kama haiwezekani kuosha pembezoni mwa jeraha, basi atafanya udhu wake kwa utaratibu wa udhu wa bandeji.

Ii. Ikiwa Kiungo Chenye Jeraha Ni Uso Au Mkono Na Kiungo Hicho Kimewekwa Bandeji:

a. Ikiwa inawezekana kuiondoa bandeji hiyo na maji hayatamletea madhara, basi atafanya udhu wake kwa utaratibu wa kawaida.

b. Ikiwa inawezekana kuiondoa bandeji hiyo lakini maji yatamletea mad– hara, basi atafanya udhu wake kwa utaratibu wa udhu wa bandeji.

c. Ikiwa haiwezekani kuiondoa bandeji hiyo, na maji hayamletei madhara lakini jeraha lina najsi, basi atafanya udhu kwa utaratibu wa udhu wa bandeji.

d. Ikiwa haiwezekani kuiondoa bandeji hiyo, na maji hayamletei madhara na jeraha halina najsi, basi atafanya udhu kwa utaratibu wa kawai– da.

e. Ikiwa haiwezekani kuiondoa bandeji hiyo, na maji yatamletea madhara, basi atafanya udhu kwa utaratibu wa udhu wa bandeji.

Iii. Ikiwa Kiungo Chenye Jeraha Ni Kichwa Au Mguu:

a. Ikiwa inawezekana kupaka sehemu isiyo na jeraha, basi atapaka na udhu wake utakuwa sahihi.

b. Ikiwa haiwezekani kupaka sehemu yoyote ile, na kupaka kutamletea madhara, basi atafanya udhu kwa utaratibu wa udhu wa bandeji.

c. Ikiwa haiwezekani kupaka sehemu yoyote nyingine, na kupaka hakumletei madhara, basi ikiwa jeraha halina bandeji atafanya udhu kwa utaratibu wa kawaida.

d. Ikiwa haiwezekani kupaka sehemu yoyote nyingine, na kupaka hakumletei madhara lakini jeraha lina bandeji, basi atafanya udhu kwa utaratibu wa udhu wa bandeji. Na atafanya ihtiyati kwa kutayammam, hivyo atafanya vyote viwili pamoja.

Kuoga

i. Ni mtu kuoga mwili wake wote kwa maji tohara na ya halali.

ii. Aina za majosho ya wajibu kisharia

iii. Josho la janaba, hedhi, istihadha, nifasi, la kumgusa maiti na la maiti.

Mambo Yanayosababisha Janaba

i. Kujamiiana, hata kama mtu hatotokwa na manii.

ii. Kutokwa na manii, sawasawa iwe usingizini au katika hali ya kuwa macho, iwe kidogo au mengi, kwa matamanio au bila ya matamanio.

Jinsi Ya Kuoga Kisharia

Kwanza: Nia, nayo ni kukusudia moyoni kuwa: Ninaoga kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Pili: Unaweza kuoga kwa njia moja kati ya njia mbili:

i. Kuoga kwa mpangilio maalumu: Nao ni kuanza kuosha kichwa na shin– go, kisha upande wa kulia wa mwili wako, halafu kuoga upande wa kushoto wa mwili wako.

ii. Kuoga kwa kuzama: Nako ni kuzama katika maji mara moja ambapo mwili wako wote uenee maji.

Zingatia:

1. Wakati wa kuoga ni lazima kuondoa vizuizi vyote mwilini vinavyoweza kuzuia maji kufika kwenye ngozi.

2. Hakuna tofauti yoyote kati ya mwanaume na mwanamke katika namna ya kuoga.

3. Kuoga kwa ajili ya janaba kunatosheleza udhu.

Mas'ala Mbalimbali

Mtu akiwa na janaba, hedhi au mfano wa hayo, ni haramu kwake mambo yafuatayo:

i. Kuswali: Lazima aoge ili Swala yake iwe sahihi, isipokuwa Swala ya maiti.

ii. Kuizunguka Al–Kaaba iliyopo mji mtukufu wa Makka.

iii. Kuyagusa maandishi ya Qur'an Tukufu.

iv. Kusoma Aya zenye sijda ya wajibu zilizopo kwenye sura nne:

1. **Sura As-Sajdah: 14.**

2. **Sura Fusswilat: 36.**

3. **Sura An-Najmi: 61.**

4. **Sura Al-Alaq: 18.**

v. Kukaa katika misikiti na makaburi ya Maimamu (a.s), na kuingia msik- iti mtukufu wa Makka na msikiti wa Mtume (s.a.w.w.) uliopo Madina.

vi. Kuweka kitu chochote msikitini.

1. Istibrau ni kitendo cha mwanaume kukamua tupu yake baada ya haja ndogo ili kuondoa mabaki ya mkojo katika njia yake. Kwa ufafanuzi zaidi tazama vitabu vikubwa vya hukmu- Mhariri.

Kutayammam

Mwenyezi Mungu asema: "Na mkiwa wagonjwa au safarini, au mmoja wenu ametoka chooni au mmeingiliana na wanawake, na hamkupata maji, basi tayamamuni mchanga ulio safi."[1]

Wakati Gani Tunatayammam?

i. Yanapokosekana maji ya kutosha kwa ajili ya udhu, au kuoga josho la kisharia.

ii. Tunapohofia kuwa kuyafikia maji kutatusababishia madhara juu ya nafsi, au mke na watoto au mali yenye kufungamana nasi.

iii. Ikiwa kuyapata maji au kuyatumia kutasababisha tabu na mashaka makubwa, ikiwemo madhila na uvunjifu wa heshima.

iv. Ufinyu wa muda katika kutafuta maji au kuyatumia kwa kiasi kwamba muda wa Swala utatupita.

v. Iwapo maji yatatosheleza tu kuondosha najisi mwilini na kwenye mavazi.[2]

Tutatayammam Kwa Kutumia Vitu Gani?

i. **Udongo na mchanga.**

ii. **Mawe na miamba.**

iii. **Changarawe, na vinginevyo vinavyoitwa ardhi.**

Masharti Ya Kusihi Kwa Tayammam

i. Nia, anuie moyoni: Ninatayammam badala ya udhu kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

ii. Tayammam ifanyike kwa vitu ambavyo inaruhusiwa kisharia kufanyia tayammam, kama vile udongo na miamba.

iii. Vitu vya kufanyia tayammam viwe tohara. iv. Vitu hivyo viwe vya halali.

iv. Viungo vya tayammam viwe tohara.

v. Kisiwepo kizuizi chochote kwenye viungo vya tayammam kama vile pete na vinginevyo.

vi. Kuzingatia utaratibu baina ya viungo vya tayammam.

vii. Afanye tayammam yeye mwenyewe na asifanyiwe na mtu mwingine isipokuwa katika hali ya dharura.

Vitenguzi Vya Tayammam:

Vitenguzi vya udhu hutumika kama vitenguzi vya tayammam, zaidi ya hapo ni kutoweka kwa udhuru uliyosababisha kufanyika kwa tayammam hiyo.

Jinsi Ya Kufanya Tayammam:

Kwanza: Nia, nayo ni kukusudia moyoni kuwa: Ninatayammam badala ya udhu au josho kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Pili: Kupiga mara moja juu ya ardhi kwa vitanga viwili, kama inavyoonekana katika picha nambari 13.

Tatu: Kupaka paji la uso kwa kutumia viganja viwili, kuanzia kwenye maoteo ya nywele mpaka kwenye nyusi pamoja na upande wa juu wa pua, na ni lazima kupaka kuanzia juu kwenda chini, kama inavyoonekana katika picha nambari 14 na 15.

Nne: Kupaka juu ya kitanga cha mkono wa kulia kwa kutumia kitanga cha mkono wa kushoto kuanzia kwenye kiwiko mpaka kwenye ncha za vidole, na lazima kupaka kuanzia juu kwenda chini, kama inavyoonekana katika picha nambari 16 na 17.

Tano: Kupaka juu ya kitanga cha mkono wa kushoto kwa kutumia kitanga cha mkono wa kulia kuanzia kwenye kiwiko mpaka kwenye ncha za vidole, na lazima kupaka kuanzia juu kwenda chini, kama

inavyoonekana katika picha nambari 18 na 19.

Mas'ala Mbalimbali Kuhusu Tayammam:

i. Ni wajibu kupiga juu ya ardhi, wala haitoshi kuweka tu mkono juu yake.

ii. Haisihi kutayammam kwa ajili ya faradhi ambayo bado wakati wake haujaingia.

iii. Tukitayammam kwa ajili ya Swala ambayo tayari muda wake umeshaingia na ikawa tayammam yetu haijatenguka wala udhuru uliyotusababisha tutayammam haujatoweka; hali hiyo ikaendelea mpaka ukaingia wakati wa sala nyingine, basi hapo tunaruhusiwa kusali Swala hii ya sasa kwa tayammam hiyo, madamu tu tunajua kuwa udhuru hautotoweka mpaka mwisho wa wakati.

Akitayammam badala ya josho, kisha akapatwa na hadathi ndogo, basi kwa mujibu wa ihtiyati atatakiwa kutayammam tena upya badala ya josho kisha achukuwe udhu, kama itawezekana. Kama haiwezekani basi atatayammam mara ya pili badala ya udhu.

1. Sura Al-Maidah: 6
2. Hizi tulizozitaja ni sababu muhimu na wala si zote, hivyo atakaye ufafanuzi zaidi arejee vitabu vya hukumu za sharia.

Swala

i. **Swala za wajibu**

ii. Swala za kila siku

iii. Swala ya kutufu Al-Kaaba

iv. Swala ya misukosuko, nayo husaliwa pale panapotokea matukio ya kiasili, kama vile, kupatwa kwa mwezi, kupatwa kwa jua, na tetemeko la ardhi.

v. Swala ya kulipa anayoisali mtoto mkubwa baada ya kifo cha baba ambaye hakutekeleza Swala za wajibu.

vi. Swala ambayo huwa wajibu kwa sababu ya nadhiri au mfano wake au kukodishwa.(ijara)

vii. Swala ya maiti.

Swala Za Kila Siku Na Idadi Ya Rakaa Zake

Nazo ni sala za faradhi ambazo ni wajibu kuzisali kila siku.

i. **Swala ya Subhi, ina rakaa mbili.**

ii. **Adhuhuri, ina rakaa nne.**

iii. **Alasiri, ina rakaa nne.**

iv. **Magharibi, ina rakaa tatu.**

v. **Isha, ina rakaa nne.**

Mavazi Ya Mwenye Kusali

Mwanamume: Ni linalositiri tupu mbili, yaani kwa kiwango cha kuweza kusitiri utupu wa mbele na wa nyuma.

Mwanamke: Lazima kwa mwanamke kusitiri mwili wake wote wakati wa Swala isipokuwa uso na vitanga vya mikono pamoja na nyayo mbili, kama inavyoonekana katika picha nambari 20.

Sharti Za Vazi La Mwenye Kusali:

i. Liwe tohara.

ii. Liwe la halali (yaani lisiwe la unyang'anyi).

iii. Vazi la mwanamume lisiwe limetengenezwa kutokana na Hariri.

iv. Lisiwe linatokana na viungo vya mzoga, ambavyo vinafikiwa na uhai, kama vile nyama ya mnyama ambaye hakuchinjwa kisharia.

v. Lisiwe linatokana na viungo vya wanyama ambao ni haramu kuliwa, hata kama watakuwa wamechinjwa kwa taratibu za kisharia, bali pia hairuhusiwi kuchukua kiasi kidogo cha viungo hivyo katika Swala.

Mas'ala Kuhusu Vazi

i. Katika hijabu ya kisharia isiyokuwa ya ndani ya Swala ni lazima kusitiri miguu, na hairuhusiwi kuvaa vazi lenye kubana wala kuonyesha mapambo.

ii. Mwanamke awapo ndani ya Sala anaruhusiwa kisharia kuvaa vazi lenye kubana au lenye kuukamata mwili na kudhihirisha mapambo iwapo tu hakuna mwanamume ajnabi anayemuona.

iii. Ni sunna kwa mwanamume katika Swala kuvaa vazi kamili kama heshima kwa sababu anasimama mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Tohara Ya Mwili

Ni sharti mwili wa mwenye kusali uwe tohara dhidi ya najisi, hata kucha na nywele, vilevile ni sharti kwa mwenye kutaka kusali awe ametawadha, na kama anatakiwa kuoga kisharia basi itamlazimu kufanya hivyo ili aweze kusali.

Najisi Zinazosameheka Katika Swala

i. Kuwapo damu ya jeraha na majipu kwenye nguo na mwili wa mwenye kusali hakudhuru Swala; mpaka litakapopona, iwapo tu haiwezekani kuiondoa au kuna ugumu wa kufanya hivyo.

ii. Pia imesamehewa kisharia damu ya jeraha na majipu iwapo kwenye mwili au nguo kama itakuwa si zaidi ya kiasi cha fundo la kidole cha shahada, madamu tu si damu ya mnyama aliye najsi, kama vile mbwa na nguruwe na kafiri, na madamu tu si damu ya mzoga, hedhi au nifasi au istihadha.

iii. Inaruhusiwa kisharia kusali na soksi, kofia, mkanda na mfano wake vilivyo najisika, miongoni mwa

vitu ambavyo havitoshelezi kusitiri tupu iwapo tukitaka kusitiri tupu mbili kwa wenyewe tu.

Masharti Ya Mahali Pa Kusalia

i. Mahali pa kusalia pawe pa halali, yaani pasiwe pa unyang'anyi.

ii. Sehemu ya kusalia iwe tulivu, yaani isiwe na mtikisiko. Sharti hili litazingatiwa katika mazingira yasiyokuwa na udhuru, ama katika hali ya udhuru kama vile msafiri wa melini au ndege, sio lazima kuzingatia sharti hili iwapo haitawezekana kuiahirisha Swala kwa kuhofia kupitwa na wakati.

iii. Sehemu ya kusalia isiwe na najisi isiyosameheka, ambayo inaweza kuhamia kwenye mwili au nguo yake.[1]

iv. Siyo sharti kwa mwanamume kumtangulia mwanamke, hasa inapokuwa kuna umbali wa kiasi cha shibri kati yao.

v. Ni lazima mahali pa kufanyia sijda pawe tohara.[2]

vi. Mahali pa kufanyia sajda pasiwe juu au chini sana kuliko sehemu ya nyayo kwa zaidi ya kiasi cha vidole vinne vilivyobebana.

Nyakati Za Swala

Mwenyezi Mungu asema: "Simamisha Swala jua linapopinduka mpaka giza la usiku na kusoma Qur'an ya alfajri (Swala ya alfajri)."[3] Na akasema: "Hakika Swala kwa wenye kuamini imekuwa ni faradhi yenye kuwekewa wakati maalumu."[4]

Imepokewa kutoka kwa Imam As-Sadiq (a.s.) kuwa: "Hakika Mtume (s.a.w.w.) alisali Adhuhuri na Alasiri kwa adhana moja na ikama mbili, na akasali Magharib na Isha pasipokuwa na safari wala ugonjwa kwa adhana moja na ikama mbili."[5]

Wakati wa Sala ya Subhi: Huanzia kuchomoza kwa alfajiri na hukomea wakati wa kuchomoza jua.

Wakati wa Swala ya Adhuhuri: Huanzia wakati jua linapopinduka wakati wa mchana mpaka kabla ya jua kuzama kwa kiasi cha muda utoshao kutimiza Swala ya Alasiri.

Wakati wa Sala ya Alasiri: Huanzia baada ya kupinduka jua baada tu ya kiasi cha kuweza kutimiza Sala ya Adhuhuri, na hukomea wakati wa kuzama jua kisharia.

Wakati wa Swala ya Magharibi: Huanza baada ya kuzama jua kisharia mpaka kabla ya nusu ya usiku kabla haujaisha muda utoshao kusali Sala ya Isha.

Wakati wa Swala ya Isha: Huanzia tangu kuzama jua kisharia pale unapopita muda utoshao kusali Sala

ya Magharib, na hukomea nusu ya usiku, na iliyo bora kwa yule ambaye alichelewa kusali sala za Magharib na Isha mpaka nusu ya usiku, azisali mpaka wakati wa kuingia alfajiri kwa lengo la kutekeleza wajibu.

Kibla

Mwenyezi Mungu asema: “Basi elekeza uso wako upande wa Msikiti Mtukufu. Na popote mtapokuwa zielekezeni nyuso zenu upande huo.”6

Ni lazima kwa mwenye kusali aelekee Kibla wakati wa Sala zote. Kibla ni upande wa Kaaba Tukufu kulingana na miji yote, hivyo Kibla hutofautiana kati ya mji na mji kulingana na tofauti za maeneo.

Wakati huo tunaelekea upande wa nyumba ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuzielekeza nyuso zetu upande wa Al-Kaaba Tukufu iliyojengwa na Nabii Ibrahim (a.s) na mwanaye Ismail (a.s).

Adhana

Imepokewa kuwa: “Malaika wasikiapo adhana kutoka duniani husema: “Hizi ni sauti za umma wa Muhammad (s.a.w.w.) wakimpwekesha Mwenyezi Mungu”, hivyo huwaombea maghfira mpaka mwisho wa Swala hiyo.”7

Kuingia wakati wa Swala hutambulishwa kwa Adhana.8 Nayo ni katika sunna zilizotiliwa mkazo wakati wa sala tano, nayo ni:

اللهُ أَكْبَرُ

Allahu Akbar (*mara nne*)
***Allah ni mkubwa* (*zaidi ya kusifiwa*).**

أَشْهَدُ أَنْ الاَ اِلهَ اِلّا الله

As-Sh’hadu an’lailaha illa llah (*mara mbili*)
Nashuhudia kuwa hakuna Mungu ila Allah tu

أَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدا رَسُوْلُ ا لله

As-Sh’hadu anna Muhammada Rasulullah (mara mbili)
Nashuhudia ya kwamba Muhammad ni Mtume wa Allah.

حَيَّ عَلَي الصَلَاة

Hayya a'las–Swalah (*mara mbili*)
Njooni kwenye Swala

حَيَّ عَلَي الفَالاَح

Hayya alal–Falah (*mara mbili*)
Njooni kwenye njia ya salama na mafanikio.

حَيَّ عَلَي خَيْر العَمَل

Hayya ala khayril–A'mal (*mara mbili*)
Njooni kwenye amali bora zaidi

اللهُ أَكْبَرُ

Allahu Akbar (mara mbili)
Allah ni mkubwa (***zaidi ya kusifiwa***)

لاَ اِله اِ لاَّ ا لله

La Ilaha Ila llah (*mara mbili*)
Hakuna Mungu ila Allah tu.

Kukimu

Baada ya kusikia sauti ya adhana, mwenye kusali hujiandaa kwa ajili ya Swala na kuelekea msikitini au mahali pengine palipoandaliwa kwa ajili ya sala ya jamaa au ya mtu mmoja mmoja ili apate kusali, na wakati huo, wakati wa kutaka kusali, huanza kukimu Swala. Nako ni katika sunna zilizotiliwa mkazo wakati wa Swala tano, atasema:

اللهُ أَكْبَرُ

Allahu Akbar (*mara mbili*)
Allah ni mkubwa (***zaidi ya kusifiwa***)

أشْهَدُ أنْ الاَ اِلهَ اِلّا الله

As-Sh'hadu an'lailaha illa llah (*mara mbili*)
Nashuhudia kuwa hakuna Mugu ila Allah tu.

أشْهَدُ أنَّ مُحَمَّدا رَسُوْلُ ا لله

As-Sh'hadu anna Muhammada Rasulullah (*mara mbili*)
Nashuhudia ya kwamba Muhammad ni Mtume wa Allah.

حَيَّ عَلَي الصَلَ ة

Hayya alas-Swalah (*mara mbili*)
Njooni kwenye Swala.

حَيَّ عَلَي الفَالاَح

Hayya alal-Falah (*mara mbili*)
Njooni kwenyenjia ya salama na mafanikio.

حَيَّ عَلَي خَيْر العَمَل

Hayya ala khayril-Amal (*mara mbili*)
Njooni kwenye amali bora zaidi.

قدْ قاَ مَتْ ا الصَلَاة

Qad qamatis-Swalah (*mara mbili*)
Hakika Swala imesimama.

اللهُ أكْبَرُ

Allahu Akbar (*mara mbili*)
***Allah ni mkubwa* (*zaidi ya kusifiwa*)**

لاَ اِلٰه اِ لاَّ ا لله

La Ilaha Ilallaha (*mara mbili*)
Hakuna Mungu ila Allah tu.

Mas'ala Kuhusu Adhana Na Iqama

i. Ni sunna katika adhana na ikama baada ya kipengele cha tatu kuongeza kipengele "As-Sh'hadu anna Aliyyan waliyullah." Kipengele hiki si sehemu ya adhana lakini ni sunna ya adhana.

ii. Adhana huachwa katika sala ya pili pale mwenye kusali anapoamuwa kukusanya kati ya Sala mbili.

iii. Adhana na ikama vyote viwili huachwa pale mwenye kusali anapoingia kwenye Sala ya jamaa ambayo tayari adhana yake imeshaadhiniwa na ikama kukimiwa. Na pia pale mwenye kusali atakapomsikia mwingine kaadhini na kukimu, kwa sharti tu kati ya adhana na Sala au ikama na sala kusiwe na muda mrefu, na pia awe amesikia vipengele vyote vya adhana na iqama.

Masharti Ya Dhana Na Iqama

i. Nia, nayo ni kunuwia kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu. Ni lazima nia hiyo idumu mpaka mwisho wa adhana

ii. Akili na imani: Mwadhini awe balehe mwenye akili timamu

iii. Adhana ya Sala ya wanaume ni lazima iadhiniwe na mwanamume.

iv. Utaratibu: Ni lazima ianze adhana na kisha ndio ikama. Na pia ni lazima vipengele vyao viwe katika utaratibu uliyotajwa bila kutanguliza wala kuchelewesha.

v. Mfululizo: Ni lazima kusiwe na kitenganishi cha wakati mrefu kati ya kipengele na kipengele.

vi. Iwe kwa kiarabu fasaha.

vii. Iwe baada ya wakati husika kuingia.

Mambo Ya Wajibu Katika Swala

i. Wajibu uliyo nguzo: Nao ni tendo ambalo huvunja Swala likiongezwa au kupunguzwa kwa makusudi au kwa kusahau.

ii. Wajibu usiyo nguzo: Nao ni tendo ambalo huvunja Sala iwapo likiongezwa au kupunguzwa kwa makusudi.

Mambo Yaliyo Wajibu Yaliyo Nguzo

i. Nia.

ii. Takbira ya kuhirimia.

iii. Kisimamo kwa ajili ya nia na kwa ajili ya takbira ya Ihraam. Na kisi– mamo ambacho huwa tu kabla ya kwenda rukuu.

iv. Rukuu.

v. Sijda mbili kwa pamoja.

Mambo Yaliyo Wajibu Yasiyo Nguzo:

i. Kusoma Alhamdu na sura kamili katika rakaa mbili za mwanzo, na kusoma Alhamdu au kusoma Tasbihi nne katika rakaa ya tatu na ya nne.

ii. Dhikri katika rukuu na sijda.

iii. Tashahhud.

iv. Swalamu.

v. Utaratibu

vi. Mfululizo.

Nia:

Nayonikukusudia kusali, nautasema: ninasali sala ya alfajiri {au adhuhuri au laasir au magharibi au isha} kwahali yakutekeleza waajibu kwakutaka radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu. na wala si lazima katika nia kutamka.bali utashi wa kimoyo unatosha. na vilevile ni sharti nia hiyo iwe ya ikhlasi, na kuainisha iana ya sala (wajibu au sunna, pungufu au timamu).

Takbira Ya Kuhirimia:

Nayo ni kusema: **“Allahu Akbar”**

Ambapo ni lazima isomwe katika hali ya kusimama na kunyooka, akiwa ameelekea kibla, vilevile ni lazima kuwa katika hali ya utulivu wa kimwili kabla ya kuitamka.

Kisomo:

i. Ni lazima kusoma Sura Alhamdu pamoja na sura nyingine yoyote kamili katika rakaa mbili za mwanzo, ama katika rakaa ya tatu na ya nne ni hiyari kusoma Alhamdu tu au Tasbihi nne:

سُبْحَانَ الله وَ الحَمْدُ لِلَهِ وَ لاَ اِلهَ اِلّا لله وَا لله أَكْبَر

"Utakasifu ni wa Mwenyezi Mungu na kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, hapana Mola wa haki ila Allah, na Mwenyezi Mungu ni Mkubwa {zaidi ya kusifiwa}."

ii. Ni lazima kujifunza namna sahihi ya kusoma katika kutamka herufi na irabu.

iii. Ni lazima kutodhihirisha kisomo katika sala za Adhuhuri na Alasiri, pia ni lazima kudhihirisha sauti katika sala za Asubuhi na Magharibi na Isha kwa wanaume pekee, ama wanawake, sio lazima kwao kudhihirisha.

iv. Swala hubatilika iwapo mtu kwa makusudi ataacha kudhihirisha sauti pale panapotakiwa kudhihirisha au kinyume chake, aidha kama itakuwa ni kwa kusahau, basi hakuna tatizo katika sala yake.

v. Ni lazima kutodhihirisha sauti wakati wa kusoma Tasbihi nne, na wakati wa kusoma Alhamdu badala yake, na vilevile katika sala ya ihtiyaat.

vi. Katika maeneo ya kutodhihirisha sauti ni sunna kudhihirisha Bismillahi isipokuwa katika rakaa ya tatu na ya nne inaposomwa sura Alhamdu badala ya Tasbihi nne.

vii. Sura za Al-Fiil na Quraysh huhesabiwa kama sura moja, halikadhalika sura za Ad-Dhuhaa na Inshiraah huhesabiwa kama sura moja.

Zingatia:

a. Kipimo cha kudhihirisha na kutodhihirisha sauti ni kusikika au kutosikika sauti.

b. Ni lazima uwepo mfululizo kati ya herufi za neno. Kama ambavyo ni lazima mfululizo huo uwepo kati ya maneno ya Aya na kati ya Aya za sura, kwa namna ambayo itasadikika kweli kuwa hili ni neno moja au Aya moja au sura maja.

c. Ni karaha kuacha kusoma Sura Ikhlasi ndani ya sala tano za faradhi.

d. Ni lazima kusoma Bismilahi mwanzo wa kila sura isipokuwa sura At-Tawba.

e. Inatosha kusoma Tasbihi nne mara moja, na ni sunna kuzisoma mara tatu katika rakaa ya tatu na ya nne kabla ya kufanya rukuu, nazo ni: **"Subhanallah, walhamdulillah, walailaaha illa llah, wallahu**

akbar”.

f. Na ni wajibu kutodhihirisha sauti wakati wa kusoma Tasbihi nne.

g. Vilevile inawezekana kwa mwenye kusali kusoma sura Alhamdu badala ya Tasbihi nne, na iliyo bora kwa imamu ni kusoma Alhamdu na maamuma asome Tasbihi nne.

Rukuu:

Mwenyezi Mungu asema: “Enyi mlioamini! Rukuuni na sujuduni na mwabuduni Mola wenu na fanyeni mema ili mpate kufaulu.”9

i. Ni lazima kufanya rukuu mara moja katika kila rakaa ya Sala.

ii. Ni lazima kuinama katika rukuu mpaka mikono ifike kwenye magoti. iii. Ni lazima katika rukuu kusoma dhikri ifuatayo: **“Sub’hana rabbiyal Adhiim wabihamdihi”** mara moja. Au **“Sub’hanallah”** mara tatu.



iii. Baada ya rukuu na kabla ya kwenda kusujudu ni lazima kusimama kwa unyoofu, ambapo ni lazima kuwa na utulivu ndani yake.

iv. Ni lazima kuwapo na utulivu wakati wa kusoma dhikri za ndani ya sala. vi. Ni sunna wakati wa kuinuka kutoka kwenye rukuu kusema: **“Samiallahu liman hamidah”.**

Sijda:

i. Ni lazima kusujudu mara mbili katika kila rakaa ya Sala.

ii. Ni lazima kuegemea viungo saba vya sijda katika hali ya kusujudu, navyo ni paji la uso, viganja viwili, magoti na vidole gumba vya miguu.

iii. Katika kila sijda ni lazima kusoma dhikri ifuatayo: **“Sub’hana rabbiyal’ aala wabihamdihi”** mara moja. Au **“Subhanallah”** mara tatu.

iv. Sehemu ya kuweka paji la uso ni lazima ilingane na ile ya kuweka miguu, na sio tatizo iwapo moja wapo itakuwa juu ya nyingine kwa kiasi cha vidole vinne vilivyobebana.

v. Ni lazima kuwa katika hali ya kutulia wakati wa kusoma dhikri ya sijda. vi. Ni lazima kukaa baina ya sajda mbili kwa hali ya utulivu, na ni sunna

vi. Wakati wa kuinuka kutoka kwenye sijda kusema: **"AllahuAkbar"**.

Masharti Ya Mahali Pa Kufanyia Sijda:

i. Sehemu ya kuwekea paji la uso ni sharti iwe ni sehemu inayoweza kuitwa ardhi, kama vile udongo au jiwe au changarawe, au miongoni mwa viotavyo ardhini, kama vile mimea kwa sharti isiwe inatumiwa kwa chakulana mavazi.

ii. Sehemu ya kuweka paji la uso ni sharti liwe na utulivu wakati wa kufanya sijda.

iii. Ni sharti sehemu hiyo iwe tohara.

Kunuti:

Ni katika sunna zilizotiliwa mkazo kukunuti katika rakaa ya pili kabla ya kufanya rukuu, nako ni maombi yoyote yanayokusudiwa ndani yake mambo ya kheri hapa duniani na akhera na hasa kuwaombea waumini.

Miongoni mwa dua ambazo ni sunna kuzisoma kama kunuti ni:

"Mola wetu! Usizipotoshe nyoyo zetu baada ya kutuongoza na utupe rehema itokayo Kwako, hakika Wewe ndiye Mpaji Mkuu."[10]

"Mola wetu! Utupe wema duniani na wema katika Akhera na utulinde na adhabu ya moto."[11]

Tashahhud:

Tashahud ni wajibu katika rakaa ya pili baada ya kufanya sijda mbili, na pia katika rakaa ya mwisho ya kila sala, kwa kusema:

أشْهَدُ أنْ لَا إلهَ إلّا الله وَحْدَةُ لَا شَرِيْكَ لَهُ وَأشْهَدُ أنَ مُحَمَّدًا عَبْدُةُ وَرَسُوْلُهُ.

اللهم صَلَّ عَلَي مُحَمَدٍ وَ اَلِ مُحَمَدٍ.

"Ashhadu an lailaha illa llahu wahdahu la shariikalahu, waashhadu anna Muhammadan abduhu

warasuuluhu, Allahumma swalli ala Muhammadin waali Muhammadin".

Dhikri ya tashahhud lazima isomwe katika hali ya kukaa na kunyooka na utulivu.

Kabla ya tashahhud ni sunna kusema: "Alhamdulillah" au "Bismillah wabillah, walhamdulillah, wakhayrul-asmai lillah".

Kutoa Salamu:

Swalam ni wajibu katika rakaa ya mwisho baada ya tashahhud, ambapo kwayo, hupata kuhalalika matendo yaliyo nje ya sala, tamko lake ni kama ifuatavyo:

السَلَامُ عَلَيْكَ أيَّهَا النَبِيُ وَرَحْمَةُ الله وَبَرْكَاتُهُ

As-Salaam Alayka Ayyuhan-Nabiyyu Warahmatullahi Wabarakatuhu.

السَلَامُ عَلَيْنا وَعَلَي عِبَادِ الله الصَالِحِيْنَ

As-Salaam alayna waala ibaadillahi As-Swalihiin.

السَلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ الله وَبَرْكَاتُهُ

As-Salaam alaykum warahmatullah wabarakatuhu.

Zingatia:

i. Iliyo wajibu ni moja kati ya salam mbili: Ya pili au ya tatu. Ama ya kwanza yenyewe ni sunna.

ii. Ni lazima kusoma salam katika hali ya kukaa, kunyooka na kutulia. iii. Ni sunna kukaa mkao wa tawarruki. 12

Mfululizo:

Nao ni muda kati ya kitendo kimoja na kingine kati ya vitendo vya sala usiwe mrefu sana kiasi cha kuiharibu sala.

Utaratibu:

Ni wajibu kufuata utaratibu katika vitendo vya sala kwa kuanza takbira ya kuhirimia kabla ya kisomo, na

Alhamdu kabla ya sura kamili, na sura kabla ya rukuu, na rukuu kabla ya sijda na kuendelea, hivyo mwenye kutanguliza kitendo kinachofuatia kabla ya kitendo kinachotangulia, au nguzo inayofuatia kabla ya ile inayotangulia, basi sala yake itakuwa batili.

Namna Ya Kusali

Baada ya Adhana na kukimu, ambavyo ni sunna zilizotiliwa mkazo kuzifanya kabla ya sala, huanza matendo yafuatayo:

1. **Nia:** Ni kukusudia moyoni kufanya tendo la sala kama ifuatavyo: Ninasali faradhi ya sala ya Subhi au Dhuhri au Alasiri au Maghrib au Isha kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Si lazima kuitamka bali kusudio la moyoni linatosha.

2. **Takbira ya kuhirimia:** Yenyewe husomwa mara baada ya nia kwa kusema **"Allahu Akbar".** Ambapo ni sunna kuinua mikono mpaka usawa wa masikio, ni lazima uanzaji wa kuinua mikonouende sanjari na uanzaji wa tamko, na umalizike sanjari na tamko hilo,

3. **Kisomo:** Nako ni kusoma katika rakaa mbili za mwanzo sura Alhamdu kisha sura nyingine kamili kama vile sura Ikhlas au yoyote ile, ukiwa katika hali ya kusimama na mnyoofu,

4. **Rukuu:** Baada ya kumaliza kisomo, inama kwa ajili ya rukuu na useme: **"Sub'hana rabbiyal Adhiim wabihamdihi**," kama inavyoonekana katika picha.



5. Baada ya hapo, inua kichwa chako toka kwenye rukuu usimame ukiwa mnyoofu, kisha useme: **"Samiallahu liman hamidah"** kama inavyoonekana katika picha. Kisha utasubiri kidogo kabla ya kwenda kusujudu.

6. **Sijda mbili:** Baada ya kutoka kwenye rukuu, tunaporomoka kwenda kusujudu kwa kuweka viungo saba vya sijda juu ya ardhi na kusema: **"Sub'hana rabiyal-Aala wabihamdihi",** Kisha tunainua kichwa kutoka kwenye sijda ya kwanza na kutulia kidogo, kisha tunasema: **"Allahu Akbar".** Kisha tunakwenda kusujudu kwa mara nyingine kwa kufanya kama tulivyofanya katika sijda ya kwanza na kusoma tuliyosoma katika sijda ya kwanza, kama inavyoonekana katika picha.

7. **Rakaa ya pili na kunuti:** Baada ya sijda ya pili katika rakaa ya kwanza, tunasimama wima kwa unyoofu kwa ajili ya kuanza rakaa ya pili, kisha tunasoma sura Alhamdu pamoja na sura kamili nyingine yoyote ile, kama tulivyofanya katika rakaa ya kwanza, kisha tunainua mikono na kuomba dua yoyote ile, au zile zilizopendekezwa.

8. **Tashahhud:** Kisha baada ya kunuti tunarukuu kama tulivyorukuu katika rakaa ya kwanza, kisha tunainuka toka kwenye rukuu na kusimama wima kwa unyoofu kama rakaa ya kwanza, ndipo tunafanya sijda mbili kama tulivyofanya katika rakaa ya kwanza, kisha baada ya sijda mbili tunakaa kwa ajili ya tashahhud na kusema:

أشْهَدُ أنْ لَا إلهَ إلّا الله وَحْدَهُ لَا شَرِيْكَ لَهُ وَأشْهَدُ أنَ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُوْلُهُ.

اللهم صَلَّ عَلَي مُحَمَدٍ وَ اَلِ مُحَمَدٍ.

"Ashhadu an lailaha illa llaha wahdahu la shariikalahu, waashhadu anna Muhammadan abduhu warasuuluhu, Allahumma swalli ala Muhammadin waali Muhammadin"

Vilevile ni lazima kufanya tashahhud katika rakaa ya mwisho ya kila sala.

9. **Tasbihi nne au sura:** Baada ya Tashahuud tunasimama wima kama mwanzo kwa ajili ya rakaa ya tatu, na hapo tutasoma sura Alhamdu peke yake au tasbihi nne kwa kusema: **"Subhanallah, walhamdulillah, walailaaha illa llah, wallahu akbar"** mara moja na vizuri zaidi ni mara tatu

10. **Kutoa Salaam:** Baada ya kumaliza tasbihi nne au sura Alhamdu, tunafanya rukuu na kisha kusujudu kama tulivyofanya katika rakaa ya kwanza, kisha tutasimama kwa ajili ya rakaa ya nne na kufanya kama tulivyofanya katika rakaa ya tatu kwa kusoma sura Alhamdu au tasbihi nne, na kisha kurukuu na kufanya sijda mbili na kukaa kitako kwa ajili ya tashahhud, na kisha tutatoa salaam kwa kusema:

السَلَامُ عَلَيْكَ أيَّهَا النَبِيُ وَرَحْمَةُ الله وَبَرْكَاتُهُ

As-Salaam Alayka Ayyuhan-Nabiyyu Warahmatullahi Wabarakatuhu.

السَلَامُ عَلَيْنا وَعَلَي عِبَادِ الله الصَالِحِيْنَ

As-Salaam alayna waala ibaadillahi As-Swalihiin.

السَلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ الله وَبَرْكَاتُهُ

As-Salaam alaykum warahmatullah wabarakatuhu.

Ufafanuzi:

Utaratibu tuliouelezea ni wa Sala ya rakaa nne, kama vile Adhuhuri, Alasiri na Isha.

Ama kwa upande wa Sala ya rakaa mbili kama vile Subhi, baada ya kumaliza tashahhud katika rakaa ya pili atasoma salam na kumaliza Sala.

Ama kama Sala itakuwa ya rakaa tatu, kama vile sala ya Maghribi, baada ya kumaliza tashahhud katika rakaa ya pili atasimama wima mnyoofu kwa ajili ya rakaa ya tatu, na baada ya kumaliza rukuu na sijda mbili, atafanya tashahhud na hatimaye atatoa salaam, hapo atamaliza Sala yake.

Vibatilishi Vya Sala:

i. Chochote kinachotengua udhu miongoni mwa vitenguzi vyake, kama vile kutokwa na mkojo au upepo.

ii. Kula na kunywa.

iii. Kucheka kwa sauti kwa makusudi.

iv. Kila kinachofuta sura ya Sala kwa makusudi au kusahau, kama vile kucheza na kupiga makofi.

v. Kugeuka sana kutoka kwenye uelekeo wa Kibla, kwa makusudi au kusahau.

vi. Kuzungumza kwa makusudi ndani ya sala.

vii. Kufunga mikono makusudi, nako ni kuuweka mmoja juu ya mwingine wakati wa hali ya kisimamo.

viii. Kulia makusudi kwa ajili ya jambo la kidunia, na wala hakuna tatizo kulia kwa jambo la Akhera.

ix. Kubatilika moja ya masharti ya Sala ukiwa tayari ndani ya sala.

x. Kutilia shaka katika idadi ya rakaa za Sala za Subhi na Maghrib, halikadhalika kutilia shaka katika rakaa mbili za mwanzo katika sala yenye rakaa nne.

xi. Kutilia shaka katika idadi ya rakaa ambazo hazina ufumbuzi wa kisharia, kama vile kutilia shaka baina ya nne na sita.

xii. Kuongeza au kupunguza nguzo kwa makusudi au kusahau.

xiii. Kuongeza au kupunguza kwa makusudi wajibu usiyokuwa nguzo ndani ya Sala.

xiv. Kugeuka mwili wote kwa makusudi kwa namna inayomtoa katika Kibla.

xv. Kusema: “Amiin” kwa makusudi baada ya sura Alhamdu.

xvi. Kila kinachobatilisha josho, kama kutokwa na manii kwa mara nyingine.

1. Najsi huhama iwapo tu kimoja kati ya najsi au kitu husika kina unyevunyevu unaohama –Mhariri.
2. Hapa ni hata kama najsi hiyo haihami, kinyume na sharti la tatu ambalo linakomea iwapo tu najsi inahama. Kwa ufafanuzi rejea vitabu vya matendo ya kisharia –Mhariri.
3. Sura Al–Israil: 78.
4. Sura An–Nisai: 103
5. Al–Faqihi, Juz. 1.
6. Sura Al–Bqarah: 144.
7. Al–Faqihi, Juz. 1.
8. Lazima ifahamike kuwa kisharia wajibu wa kutambua uingiaji wa muda wa sala ni wa mtu binafsi, hivyo kila mmoja ana wajibu wa kujua je wakati wa Sala fulani umeingia au la. Na wala si wajibu wa mwadhini peke yake, kama ambavyo ni wajibu wa kila mmoja kujua ni upi upande wa Kibla ili aweze kuelekea huko wakati wasala yake.
9. Sura Al–Haj: 77
10. Sura Al Imran: 8.
11. Sura Al–Baqarah: 201.
12. Mkao wa tawarrukk ni mkao wakuweka matako chini bila kukalia visigino vya guu–Mhariri

Swala Ya Tahdhari (Ihtiyatwi):

i. Swala hii husaliwa ili kufidia upungufu unaodhaniwa katika idadi ya rakaa za Sala baada ya kuwa na shaka na idadi ya rakaa hizo.

ii. Ni lazima isaliwe mara tu baada ya kumaliza kusali na kabla ya kufanya mambo yabatilishayo Sala, kama vile kuzungumza na kugeuka kulia na kushoto kutoka uelekeo wa kibla.

iii. Ni lazima masharti ya Sala yakamilike ndani yake.

Namna Ya Kuisali:

Ni lazima iwepo nia, Takbira ya kuhirimia, kusoma sura Alhamdu pekee kimyakimya bila kudhihirisha sauti hata Bismillah, vilevile ni lazima kufanya rukuu, sijda mbili, tashahhud na kutoa salam, sawasawa iwe rakaa moja au mbili.

Ni Wakati Gani Tunasujudu Sijda Mbili Za Usahaulifu?:

Sijda mbili za usahaulifu huwa wajibu kwa mtu anayesali ikiwa atatokewa na moja ya mambo yafuatayo:

i. Kuzungumza katika sala kwa kusahau.

ii. Kusahau sijda moja inapopita mahali pa kuifanya.

iii. Kuacha kusoma tashahhud kwa kusahau.

iv. Kutoa salam mahali ambapo sio pa kutoa salam.

v. Kutilia shaka kati ya rakaa ya nne na ya tano akiwa katika hali ya kukaa.

Mas'ala Mbalimbali Kuhusu Sijda Mbili Za Usahaulifu:

i. Sijda mbili ni wajibu mara tu baada ya sala.

ii. Nia ni lazima katika sijda mbili za usahaulifu.

iii. Ni sunna kusoma Takbira ya kuhirimia.

iv. Hakuna rukuu katika sijda mbili za usahaulifu.

Namna Ya Kufanya Sijda Mbili Za Usahaulifu:

Zenyewe ni sijda mbili zinazosaliwa kwa kukaa, ni lazima azifanye mara tu baada ya kumaliza sala na kabla ya kufanya mambo ya nje ya sala, tena kwa kufuata utaratibu ufuatao:

a. Nia ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu.

b. Ni sunna kusoma Takbira ya kuhirimia.

c. Kusujudu: Ni sunna kusoma maneno yafuatayo:

بسْمِ الله وَبالله السَلَامُ عَلَيْكَ أَيَّهَا النَبِيُ وَرَحْمَةُ الله وَبَرْ كَا تُهُ

"Bismillahi Wabillahi, As-Swalam alayka ayyuhan-Nabiyyu warahmatullahi wabarkatuhu"

d. Kukaa katika hali ya utulivu.

e. Kusujudu mara ya pili kama awali.

f. Baada ya sijda mbili ni lazima kusoma tashahhud na kutoa salam moja kwa kusema:

الحَمْدُ لِلَه أَشْهَدُ أَنْ لَاإِلهَ إِلَّا الله وَحْدَ ةُ لَا شَرِيْكَ لَهُ وَ أَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُةُ وَرَسُوْلُهُ.

اللهم صَلَّ عَلَي مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ. السَلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ الله وَبَرْ كَاتُهُ.

"Ashhadu an lailaha illa llaha wahdahu la shariikalahu, waashhadu anna Muhammadan abduhu warasuuluhu, Allahumma swalli ala Muhammadin waali Muhammadin. As-Salam alaykum warahmatullahi wabarkatuhu."

Shaka Zinazobatilisha Sala:

i. Shaka kuhusu idadi ya rakaa za sala yenye rakaa mbili na tatu, pia shaka kuhusu rakaa mbili za mwanzo wa sala yenye rakaa nne kabla ya kakamilisha sajda mbili katika rakaa ya pili.

ii. Shaka kati ya rakaa ya pili na ya tano na kuendelea.

iii. Shaka kati ya rakaa ya tatu na ya sita na kuendelea.

iv. Shaka kati ya rakaa ya nne na ya sita na kuendelea.

Shaka Zenye Kupuuzwa:

i. Shaka katika utekelezaji wa kifungu miongoni mwa vifungu vya sala baada ya kuwa umepita mahali pake.

ii. Shaka baada ya kutoa salam.

iii. Shaka ya mtu mwenye hali ya kushakiashakia.

iv. Shaka ya Imamu au maamuma kuhusu idadi ya rakaa. Katika hali hii Imamu anaweza kuwa na uhakika wa kusali kwake na Maamuma akawa na shaka, au Maamuma akawa na uhakika lakini Imamu akawa na shaka. Katika hali hii yule mwenye shaka amfuate yule mwenye uhakika.

v. Shaka katika Sala ya Sunna. Kwani anaweza kufuata moja ya pande mbili za shaka na akakamilisha Sala yake.

Jedwali Ya Maasumina Kumi Na Wanne.

JINA	TAREHE YA KUZALIWA	TAREHE YA KUFARIKI	ALIKOZIKWA
Mtume Muhammad bin Abdillahi (s.a.w)	Mwezi 17 Shawwal (Mfungo sita) mwaka wa 52 kabla ya Hijrah	Mwezi 28 Safar (Mfungo tano) mwaka wa 11 Hijiriyyah	Madina ; Saudi Arabia
Imam Ali bin Abi Talib (a.s)	Mwezi 13 Rajab mwaka wa 23 kabla ya Hijrah	Mwezi 21 Ramadhan mwaka wa 40 Hijiriyyah	Najaf; Iraq
Fatimah binti Muhammad (a.s)	Mwezi 20 Jamadil Akhar (Mfungo tisa) mwaka wa 8 kabla ya Hijrah	Mwezi 3 Jamadil Akhar (Mfungo tisa) mwaka wa 11	Madina ; Saudi Arabia
Imam Hassan bin Ali (a.s)	Mwezi 15 Ramadhan mwaka wa 3 Hijiriyyah	Mwezi 28 safar (Mfungo tano) mwaka wa 50	Madina ; Saudi Arabia
Imam Hussein bin Ali (a.s)	Mwezi 3 Shabaan mwaka wa 4 Hijiriyyah	Mwezi 10 Muharram (Mfungo) mwaka wa 61 Hijiriyyah	Karbala; Iraq
Imam Ali bin Hussein (a.s)	Mwezi 5 Shabaan mwaka wa 38 Hijiriyyah	Mwezi 25 Muharram (Mfungo nne) mwaka wa 95 Hijiriyyah	Madina ; Saudi Arabia
Imam Muhammad bin Ali (a.s)	Mwezi 1 Rajab mwaka wa 57 Hijiriyyah	Mwezi 7 Dhul-hijja (Mfungo tatu) mwaka wa 114 Hijiriyyah	Madina ; Saudi Arabia
Imam Ja'far bin Muhammad (a.s)	Mwezi 17 Rabiul-Awwal (Mfungo sita) mwaka wa 83 Hijiriyyah	Mwezi 25 Shawwal (Mfungo mosi) mwaka wa 148	Madina ; Saudi Arabia
Imam Musa bin Ja'far (a.s)	Mwezi 6 Safar(Mfungo tano) mwaka wa 128 Hijiriyyah	Mwezi 25 Rajab mwaka wa 183 Hijiriyyah	Kadhimiyyah; Iraq
Imam Ali bin Musa (a.s)	Mwezi 11 Dhul-Qada (Mfungo pili) mwaka wa 148 Hijiriyyah	Mwezi 29 Safar (Mfungo tano) mwaka wa 203 Hijiriyyah	Khurasaan; Iran
Imam Muhammad bin Ali (a.s)	Mwezi 10 Rajab mwaka wa 195 Hijiriyyah	Mwezi 29 Dhul-Qada (Mfungo pili) mwaka wa 220	Kadhimiyyah; Iraq
Imam Ali bin Muhammad (a.s)	Mwezi 2 Rabil-Akhar (Mfungo saba) mwaka wa 212 Hijiriyyah	Mwezi 3 Rabiul-Awwal (Mfungo Sita) mwaka 254 Hijiriyyah	Samarraa; Iraq
Imam Hassan bin Ali (a.s)	Mwezi 8 Rabil-Akhar (Mfungo saba) mwaka wa 232 Hijiriyyah	Mwezi 8 Rabiul-Awwal (Mfungo Sita) mwaka wa 260 Hijiriyyah	Samarraa; Iraq
Imam Muhammad bin Hassan Al-Mahdi (a.s)	Mwezi 15 Shaaban mwaka wa 255 Hijiriyyah	Bado yu hai na yuko katika Ghaiba kuu	

Orodha Ya Vitabu Vilivyo Chapishwa Na Al-Itrah Foundation:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka kumi na Tisa
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu

35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Maulidi
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Kuzuru makaburi
53. Umaasumu wa Manabii
54. Qur'an inatoa changamoto
55. Tujifunze misingi ya dini
56. Nahjul Balagha Sehemu ya Kwanza
57. Nahjul Balagha Sehemu ya Pili
58. Dua Kumayl
59. Uadilifu wa masahaba
60. Asalaatu Khayrunminaumi
61. Sauti ya uadilifu wa binadamu
62. Umaasumu wa Mitume Sehemu ya kwanza
63 Maswali na Mishkili Elfu Sehemu ya kwanza
64. Umaasumu wa Mitume Sehemu ya tatu
65. Umaasumu wa Mitume Sehemu ya pili
66. Maswali na Mishkili Elfu Sehemu ya pili
67. Maswali na Mishkili Elfu Sehemu ya tatu
68. Malezi ya mtoto katika Uislamu.

Back Cover

Sala ni nguzo kubwa ya dini. Mtukufu Mtume (s.a.w.) amesema: "Sala ni nguzo ya dini, mwenye kuivunja ameivunja dini, na mwenye kuisimamisha ameisimamisha dini." Mtukufu Mtume ameongeza: "Kila kitu kina uso, na uso wa Uislamu ni sala. Mwenye kuacha kusali ameuchafua uso wa dini." Imam Muhammad Baqir (a.s.) amemnukuu Mtukufu Mtume (s.a.w.) akisema: "Kitu cha kwanza atakachohesabiwa muumini (Siku ya Kiyama) ni Sala. Ikikubaliwa yatakubaliwa matendo mengine, na ikikataliwa yatakataliwa matendo mengine pia."

Kwa ufupi, kuna hadithi nyingi sana kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.) na Maimamu (a.s.) kuhusu umuhimu wa Sala kiasi kwamba katika hadithi moja, Mtukufu Mtume (s.a.w.) amesema kwamba kitu chenye kutofautisha baina ya Uislamu na ukafiri ni Sala.

Wakati huu tulionao una mitihani mingi sana, vijana wa Kiislamu na wazee pia wamejitumbukiza katika vitendo viovu na vichafu kiasi kwamba mtu hawezi kumtofautisha na mnyama, na pengine hata mnyama ni afadhali. Ili kuishinda mitihani hii na maovu haya, dawa yake ni kushikamana na Sala. Allah 'Azza wa Jalla anasema katika Qur'ani Tukufu: "... Hakika Sala huzuia mambo machafu na maovu, na kwa hakika kumbuko la Allah ni (jambo) kubwa kabisa, na Allah anajua mnayoyatenda." (29:45)

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Al-Itrah Foundation
Kwa kushirikiana na:
Hafez Institute Ltd,
S.LP. 63211,
Dar-es-Salaam, Tanzania
Barua Pepe: hafezinstitute@yahoo.com [9]

Source URL: https://www.al-islam.org/sw/sala-ni-nguzo-ya-dini-mustafa-ranjbar-shirazi#comment-0

Links
[1] https://www.al-islam.org/sw/person/mustafa-ranjbar-shirazi
[2] https://www.al-islam.org/sw/organization/al-itrah-foundation
[3] https://www.al-islam.org/printpdf/book/export/html/36240
[4] https://www.al-islam.org/printepub/book/export/html/36240
[5] https://www.al-islam.org/printmobi/book/export/html/36240
[6] https://www.al-islam.org/sw/person/ibrahim-khamisi
[7] https://www.al-islam.org/sw/tags/salah-prayers

[8] mailto:ranjbar85@yahoo.com
[9] mailto:hafezinstitute@yahoo.com